

***HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA***



***SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA  
MUSOMA***

***(ADA NA USHURU WA UZOAJI, UTUPAJI TAKA NA USAFI  
WA MAZINGIRA ZA MWAKA 2017***

***SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, 1982***

***(SURA YA 290)***

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6 (1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA  
(ADA NA USHURU MBALIMBALI ) ZA MWAKA 2017**

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma (Ada na Ushuru) za mwaka 2017 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali. Jina na tarehe ya kuanza kutumika
2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa Eneo la kutumika
3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itahitajika vinginevyo:- Tafsiri ya maneno  
“Afisa Mwidhiniwa” ni mtu yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi akiwemo.  
“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.  
“Mazao” maana yake ni mazao yote ya chakula, biashara, maua, matunda na mboga yanayolimwa ndani na nje ya Halmashauri.  
“Mifugo” maana yake ni wanyama wote wafugwao na binadamu na itajumuisha nyuki, samaki, bata na kuku.  
“Mfugaji” maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji wa mifugo katika eneo la Halmashauri.  
“Mkazi” maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri, isipokua mtu;

- (a) mwenye umri chini ya miaka 18;
- (b) asiyejiweza kutokana na ulemavu, kuugua au uzee wa zaidi ya miaka sitini ambaye ni tengemezi kwa mtu mwingine;
- (c) mwanafunzi aliyeko masomoni muda wote.

**Kibali** maana yake ni idhini au ruhusa itakayotolewa na Halmashauri kwa mjibu wa sheria hizi.

**“Mkurugenzi”** inamaanisha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma au mtu yeyote atakayefanya kazi kwa niaba yake.

**“Mwalo”** eneo wanaloshushia na kupakia samaki na mizigo mingineyo ambalo linapakana na ziwa.

**“Sheria”** inamaanisha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290.

**“Soko”** Maana yake ni eneo lolote lililotengwa rasmi na Halmashauri kwa matumizi ya soko.

**“Wakala”** inamaanisha ya mtu, shirika, taasisi, kampuni au kikundi kilichoteuliwa na kupewa jukumu la kukusanya ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

- 4. (1) Italipwa ada na ushuru utakaokusanywa na Halmashauri kutoka kwa wafanyabishara kutokana na huduma na vibali vitolewavyo na Halmashauri.

- (2) Ada na ushuru vitakavyolipwa kutokana na Sheria ndogo hizi vitalipwa kuanzia tarehe 1 mwezi Julai hadi tarehe 30 Juni ambapo itakuwa siku ya mwisho ya kulipa kodi mbalimbali kwa Halmashauri katika mwaka wa fedha husika.

Ulipaji wa Ada na Ushuru

- (3) Mawakala watawasilisha fedha waliyokusanya kadri ya mikataba yao na endapo watahindiwa watakuwa wamekiuka sheria ndogo hizi.

- 5. Utakuwa wajibu wa kila mtu anayepaswa kulipa ada na ushuru kulipa kwa Afisa Mwidhiniwa au Wakala wa Halmashauri kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

- 6. (1) Kutakuwa na ada na ushuru vitakavyotozwa na Halmshauri na kulipwa na kila mfanyabiashara anayefanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmshauri. Viwango hivyo vitakuwa kama vinavyoonekana katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa Kulipa Ada na Ushuru

- (2) Kutakuwa na Ada ya kushusha na kupakia mizigo katika masoko na mialo ya Halmashauri na maeneo yote yaliyoidhinishwa na Halmashauri

- (3) Ada na ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupatiwa leseni, kibali au huduma husika na utakuwa kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Ada na ushuru

- (3) Ada na ushuru vitalipwa kadri ilivyooneshwa kwenye sehemu husika katika Jedwali la Sheria hizi.
- (4) Ada na Ushuru vilivyooneshwa katika aya ndogo ya kwanza ya Sheria Ndogo hizi vitatozwa kwa kila mtu atakayepokea huduma au kufanya biashara ndani ya mipaka ya mamlaka ya Halmashauri.
- (5) Ada na ushuru unaotozwa na Halmashauri vitalipwa kwa Halmashauri au wakala wake.
7. Kutakuwa na ada na ushuru wa mabasi makubwa, mabasi madogo, daladala na magari ya watu binafsi.
8. (1) Mtu yeyote hatonunua au kuuza au kubadilishaana bidhaa au mazao yoyote ndani ya mamlaka ya Halmashauri isipokuwa katika masoko yaliyotengwa na Halmashauri.
- (2) Kuuza, kununua au kubadilishana bidhaa kunaweza kufanyika nje ya soko kwa idhini na kibali maalumu cha maandishi cha Halmashauri au endapo kuuza, kununua au kubadilishana bidhaa kuwe kwa ajiri ya matumizi ya nyumbani.
- (3) Halmshauri inaweza kuelekeza aina fulani za mazao kuuzwa kwa mnada wa wazi, na kuwa mnada huo utakuwa kadri Halimashauri itakavyoelekeza.
9. (1) Kutakuwa na ushuru wa samaki kama ulivyobainishwa kwenye Jedwali la sheria ndogo hizi.
- (2) Ushuru wa samaki utatozwa katika mialo yote iliyo ndani ya mamlaka ya Halmshauri.
10. (1) Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote au kikundi chochote kuwa wakala wa kuikusanyia ada na ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi na mtu yeyote au kikundi kilichoteuliwa kuwa wakala kitakuwa na mamlaka ya kukusanya ada na ushuru kama Halmashauri na kinaweza kutumia mamlaka ya Halmashauri kufungua kesi ya jinai Mahakamani na baadaye kesi ya madai dhidi ya mtu yeyote au kikundi chochote kitakachoshindwa kulipa ada na ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi kwa taarifa ya awali kwa Halmashauri.
- (2) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kubatilisha uteuzi wa wakala pale itakapothibitika baada ya utafiti wa kina kuwa wakala anakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi kwa kushindwa kuwasilisha mapato ya Halmashauri.
11. Kadri ya masharti ya Sheria Ndogo hizi Afisa yoyote, Wakala au Mwajiriwa wa Halmashauri, atakuwa na mamlaka ya kuingia kwenye ardhi yoyote, jengo lolote, nyumba au chombo chochote ndani ya

Uteuzi wa Mawakala

Mamlaka ya kuingia na kukagua

mamlaka ya Halmashauri kwa lengo la kutekeleza Sheria Ndogo hizi.

12. (1) Mtu yeyote, taasisi au kikundi kilichoteuliwa na kupewa jukumu la kukusanya ushuru na bila sababu za msingi,
- Akishindwa kuleta taarifa za mapato kama zinavyoelekezwa na Sheria Ndogo hizi,
  - Akishindwa kurejesha ada na ushuru alivyokusanya baada ya muda wa kuwasilisha kupita,
  - Akishindwa kutunza taarifa zinazohusiana na ada na ushuru zitozwazo na kukusanywa,
  - Atashindwa kutoa taarifa kwa ajiri ya kufanyiwa tathmini na uthamini kadri ya maelekezo ya Sheria,
  - Akizuia au kujaribu kuzuia afisa mwidhiniwa au mkusanya mapato kutekeleza jukumu lake kadri ya mamlaka alinayo katika sheria ndogo hizi,

Makosa na Adhabu kwa mawakala wa kukusanya ushuru

Atakuwa amefanya kosa na akikutwa na hatia atatozwa faini isiyozidi kiasi cha shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote viwili kwa pamoja.

Wajibu wa kutoa taarifa

(2) Pasipo kuathiri maana ya aya ya (1) Halmashauri inaweza kurejesha ada na ushuru uliokusanywa kwa kupitia mashtaka ya jinai na mashauri ya madai.

(3) Mashauri ya madai yatakayofunguliwa mahakamani kuhusiana na madai ya ada na ushuru, yatafunguliwa kwa hati ya mkato (Summary Procedure)

13. (1) Mtu yeyote atakayetakiwa kutoa taarifa atatoa taarifa hizo kwa utashi wake na kwa kadri atakavyokuwa ametakiwa na Halmashauri kwa ajiri ya kufanya uthamini wa ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa minajiri ya kupata taarifa kama ilivyo katika aya ya (1) ya Sheria Ndogo hizi, Halmshauri inaweza kumtaka mtu yeyote kufika mbele yake kwa wakati na sehemu itakayoteuliwa.

(3) Mtu yeyote ambaye atakuwa ametakiwa kutoa taarifa katika Sheria Ndogo hizi :-

- Akikaidi au kukataa bila sababu ya kisheria, au akishindwa kutoa taarifa kama atakavyotakiwa; au
- Kwa makusudi akapotosha au kujaribu kupotosha Halmashauri katika jambo lolote linalohusiana na ukusanyaji wa ada na ushuru,

Atakuwa amefanya kosa na akikutwa na hatia atatozwa faini isiyozidi kiasi cha shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote viwili kwa pamoja.

Mamlaka ya kukagua

14. Afisa yeyote au Mwajiriwa wa Halmashauri aliyeidhiniwa kwa maandishi kwa niaba ya Halmashauri anaweza kuingia kwenye ardhi yoyote, jengo, makazi, au chombo ndani ya mamlaka kwa ajiri ya utekelezaji wa sheria

ndogo hizi atakagua au kuhitaji utekelezaji wa sheria ndogo hizi.

15. (1) Mtu yeyote, ambaye kwa namna yoyote atakuwa na wajibu wa kulipa ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi:- Makosa na Adhabu

Atapuuzua, kukataa au kushindwa kulipa ada na ushuru kama ilivyooneshwa;

- a) Akikwamisha, akishawishi au akisaidia mtu yeyote kutolipa ada na ushuru.
- b) Kwa namna yoyote akimzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake au mamlaka yake katika Sheria Ndogo hizi; au
- c) Kwa namna yoyote atakiuka Sheria ndogo hizi.

Atatenda kosa na akikutwa na hatia atatozwa faini isiyopungua kiasi cha shilingi za kitanzania laki mbili (tshs 200,000/-) na kisichozi shilingi za kitanzania milioni moja (tshs 1,000,000/-) au kifungo cha miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja na kwa nyogeza ya adhabu hizo atatakiwa kulipia ada au ushuru ambao alipaswa kulipa kwa Halmashauri.

(2) Hakuna lolote katika aya hii litakalochukuliwa kuwa linamhalalishia mtu kinga ya uzembe au kutokuwa na kumbukumbu katika utekelezaji wa majukumu yake katika Sheria ndogo.

16. Pale ambapo makosa yatafanywa na Kampuni na kuthibitika kutenda kosa, kwa ridhaa au ufahamu wa au kuchangiwa na mkurugenzi, meneja, katibu au ofisa yeyote wa kampuni, au mtu yeyote atakayetenda kwa ajiri ya Kampuni, atakuwa anatenda kosa, kampuni pamoja na watendaji wake pale itakapobidi watawajibika. Makosa kwa kampuni

17. (1) Malipo yoyote na ada au adhabu vitakavyolipwa na mtu yoyote katika Sheria Ndogo hizi yatakuwa madeni halali yatakayolipwa kwa Halmashauri na yatadaiwa kutoka kwa mtu yeyote kama shauri la madai kwa niaba ya Mkurugenzi au Afisa yeyote aliyeidhiniwa na Mkurugenzi. Kulipwa madeni

(2) Bila kupotosha ujumla wa utaratibu wa mbinu za kurejesha madeni yaliyoelezwa kwenye aya ya (1) hapa juu, pale itakapobainika kuwa mtu anadaiwa na Halmashauri, Mkurugenzi au Afisa yeyote aliyeidhiniwa na mkurugenzi atafungua hati ya madai mahakamani ikieleza kiwango cha kosa na deni linalodaiwa.

(3) Hati iliyowasilishwa mahakamani ikiridhiwa na mahakama yenye mamlaka, itakuwa amri halali ya mahakama dhidi ya mtu anaedaiwa pamoja na riba ya asilimia kumi (10%) tangu tarehe ilipotolewa hadi siku ya kulipwa kwa deni. Amri hiyo itatekelezwa kama zilivyo amri nyingine za mahakama.

(4) Kila hati itakayowasilishwa Mahakamani katika

utaratibu ulioelezwa hapa juu, itakuwa ushahidi wa ukweli wa kile kilichooneshwa katika hati hiyo.

18. Mtu yeyote atakayekiuka kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia kama hakuna adhabu maalum iliyoainishwa katika kifungu kilichokiukwa atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili tshs 200,000/-na kisichozidi shilingi za kitanzania milioni moja (tshs 1,000,000/-) au kifungo kisichopungua miezi sita jela au vyote kwa pamoja, faini na kifungo. Adhabu ya jumla
19. Pale mtu yeyote atakapokuwa ametenda kosa, mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa hilo na kumuamuru kulipa kiasi atakachoona kinafaa. Kufifilisha kosa.

## JEDWALI

### SEHEMU A

#### TOZO ZINAZOLIPWA KWA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

*Aina ya jengo*

*Ada na Ushuru vinavyotozwa*

#### **1. MAJENGO YA HALMASHURI:**

- a) Ukumbi Mkubwa wa Halmashauri ..... Tshs 400,000/= kwa siku  
b) Ukumbi Mdogo wa Halmashauri ..... Tshs 200,000/- kwa siku  
c) Majengo ya Biashara/Makazi ..... Kadri ya mkataba wa pango  
d) Vizimba /Maduka ya Biashara .....Kadri ya Mkataba wa Pango

#### **2. MITAMBO YA UJENZI**

- a) Kukodi Grader .....850,000/=kwa siku  
b) Kukodi Wheel Loader.....500,000/= kwa siku  
c) Kukodi Bulldozer – D8 .....1,200,000/= kwa siku  
d) Kukodi Bulldozer – D4 .....800,000/= kwa siku  
e) Kukodi Cesspit Empire Vehicle.....200,000/= kwa siku  
f) Kukodi medium excavator .....600,000/= kwa siku  
g) Kukodi Dump truck.....1,500,000/= kwa siku

3. **USHURU WA VIWANDA VYA MATOFARI** .....Tshs 200,000/= Kwa Mwaka

**SEHEMU B**

**ADA ZA MANCHINJIO NA MAENEO YA KUBAMBIA NA KUHFADHI NGOZI, UPANGAJI  
WA MADARAJA NA UCHUNAJI WA NGOZI**

<b>a) Eneo la Kuchinja (Slaughter house fee)</b>	<b>Ada</b>
(i) Ng'ombe .....	3,500/= kwa kichwa
(ii) Mbuzi/Kondoo .....	1,500/= kwa kichwa
(iii)Nguruwe .....	3,500/= kwa kichwa

**Ada ya kutumia jengo linalotumika kwa kubambia Ngozi ;**

Kila Mtumiaji .....Tshs 10,000/= kwa mwaka

**Ada ya leseni za wapanga madaraja (Grader's license)**

Kila mmoja .....Tshs 10,000/= kwa mwaka

**Ada ya leseni za Wachunaji (Dressor's license)**

Kila mmoja .....Tshs10,000/= kwa mwaka

**a) Ushuru wa kukagua (Inspection Fees);**

(i) Ng'ombe.....	Tshs 1,500/= kwa kichwa
(ii) Mbuzi/Kondoo.....	Tshs 800/= kwa kichwa
(iii)Nguruwe.....	Tsh 800/= kwa kichwa

**b) Ushuru wa mifugo Mnadani**

(i) Ng'ombe .....	Tshs 5,000/= kwa kichwa
(ii) Mbuzi/kondoo .....	Tshs 2,000/= kwa kichwa
(iii) Nguruwe.....	Tshs 2,000/= kwa kichwa
(iv)Kuku/Bata .....	Tshs 200/=kwa kichwa

**c) Ada ya kukusanya na kusafirisha Wanyama ;**

(i) Ndani ya Halmashauri ya Manispaa	
( ii).Ng'ombe .....	Tshs 1,000/= kwa kichwa
(ii) Mbuzi/Nguruwe/Kondoo .....	Tshs 500/= kwa kichwa
(iii) Kuku /Bata .....	Tshs 200/= kwa kichwa .

**(iv)Nje ya Halmashauri ya Manispaa**

Ng'ombe .....	Tshs 1,500/= kwa kichwa
Mbuzi/Nguruwe/Kondoo .....	Tshs 500/= kwa kichwa

**(v) Nje ya Mkoa**



Ng'ombe .....Tshs 2,500/=kwa kichwa  
Mbuji/Nguruwe/Kondoo .....Tshs 1,500/=kwa kichwa

### **SEHEMU C**

#### **USHURU WA KUSHUSHA NA KUPAKIA SAMAKI, DAGAA NA MAZAO YA ZIWANI**

##### **CHINI YA FUNGULA 6(2)**

#### **a) SAMAKI WA BICHI**

i) Ujazo na uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs 200/=kwa kila kilo

#### **b) SAMAKI WAKAVU**

(i) Ujazo na uzito kuanzia kilo kilo 1 na kuendele .....Tshs 500/=kwa kila kilo moja

(ii) Unga wa mabaki ya Samaki (Fish meal)

ujazo na uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea ..... Tshs 50/=kwa kila kilo moja

#### **c) DAGAA WA KAVU**

(i) ujazo na uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea..... Tshs 40/= kwa kila kilo moja

#### **d) DAGAA WABICHI**

i)Ujazo kuanzia kilo 1 na kuendelea.....Tshs 10/=kwa kila kilo moja

#### **e) KONOKONO**

i) Kuanzia ujazo na uzito wa kilo 1 na kuendelea .....Tshs 20/= kwa kila kilo moja

#### **f) MABONDO**

i) Mabondo mabichi kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs.1,000/=kwa kila kilo moja

ii) Mabondo makavu kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs 2,000/= kwa kila kilo moja

### **SEHEMU D**

#### **USHURU WA KUSHUSHA NA/ KUPAKIA MIZIGO SOKONI**

##### **CHINI YA FUNGULA 6(2)**

**Ada (Tshs)**

#### **UJAZO KWENYE MAGUNIA**

a) Maharage uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs 30/= kwa kila kilo moja

b) Karanga uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs 30 /=kwa kila kilo moja

c) Mahindi uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs 30 /=kwa kila kilo moja

d) Ulezi uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs 30 /=kwa kila kilo moja

e) Mchele uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs 30 /=kwa kila kilo moja

f) Uwele uzito kuanzia kilo 10 na kuendelea .....Tshs 30 /=kwa kila kilo moja

g) Tangawizi uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea ..... Tshs 30 /=kwa kila kilo moja

h) Pilipili hoho uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs 30 /=kwa kila kilo moja

i) Vitunguu maji uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs 30/= kwa kila kilo moja

j) Vitunguu swamu uzito kuanzia kilo 1 na kuendelea .....Tshs 30/=kwa kila kilo moja

## **UJAZO WA LORI /GARI LOLOTE**

i)Lori lilojaa bidhaa aina ya

Tikiti maji , Matango ,Papai ,Nanasi, Pasheni, Karoti ,

Vitunguu Bidhaa za viwandani .....Tshs 50,000/= kwa Lori /Gari moja

ii)Lori /Gari lolote lililojaa mikungu ya dizi .....Tshs 50,000/= kwa Lori /Gari

## **UJAZO WA MKOKOTENI / BAJAJI**

Mkokoteni /Bajaji iliyojaa bidhaa aina ya

Tikiti maji , Matango ,Papai ,Nanasi Pasheni

Nyanya , viazi vitamu ,vitunguu .....Tshs 10,000/= kwa kila mkokoteni /Bajaji

### **SEHEMU E**

#### **KUPAKUA MAZAO YA MALI ASILI**

- a) Gunia la mkaa..... Tshs 1,000/=
- b) Mbao, magogo, mirunda
- i) Gari kuanzia tani 1 hadi 2..... Tshs 10,000/=
- ii) Gari la kuanzia tani 3 hadi 7..... Tshs 50, 000/=
- iii) Gari la kuanzia tani 8 hadi 12..... Tshs 100,000/=
- iv) Gari la kuanzia tani 13 na zaidi..... Tshs 200,000/=

### **SEHEMU F**

#### **ADA YA VITUO VYA KUOSHEA MAGARI**

- a) Maeneo katikati ya mji .....50,000/= kwa mwezi
- b) Nje ya maeneo ya katikati ya mji .....30,000/= kwa mwezi

### **SEHEMU G**

#### **VIBALI VYA UJENZI**

#### **ADA YA MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI**

- a) Majengo
- i) Jengo la makazi la ghorofa moja .....tshs 50,000/=
- ii) Jengo la makazi la ghorofa mbili .....tshs 100,000/=
- iii) Jengo la makazi zaidi ya ghorofa moja .....tshs 500,000/=
- iv) Jengo la biashara la ghorofa moja .....tshs 100,000/=
- v) Jengo la biashara la ghorofa mbili .....tshs 200,000/=
- vi) Jengo la biashara ghorofa zaidi ya mbili .....tshs 1, 000,000/=
- Vii) Jengo la kawaida la biashara..... tshs 60,000/=
- viii) Taasisi mbalimbali..... tshs 200,000/=
- xi) Kiwanda cha kawaida .....Tshs 1, 000,000/=
- xKiwanda kikubwa ..... Tshs 1, 500,000/=

xi) Kiwanda kidogo .....	Tshs 200,000/=
xii) Nyumba ya Kawaida Kata za mjini .....	Tshs 50, 000/=
xiii) Nyumba ya Kawaida Kata za Nje ya Mji.....	Tshs 30,000/=
xiv) Ujenzi wa Minara .....	Tshs 2,000,000/=
xv) Kituo cha mafuta .....	Tshs 1,500,000/=
xvi) ujenzi wa Karakana / .....	Tshs 100,000/=
xv) Kuhuisha kibali kilichoisha muda wake .....	Nusu ya Gharama za kibali cha awali

**c) Kuvunja na kubadili jengo lililopo**

i). Kuondoa jengo lililopo na kubadili jengo .....Tshs 100,000/-

iii) Kuongeza na kubadili jengo ..... Tshs 100,000/-

**c) Ada ya Vibali vya ujenzi mwingine**

i) Sehemu ya kuoshea magari( car wash ).....Tshs.500,000/-

iii) Uzio/Fence .....Tshs.500/-kwa mita moja

b) Kuhuisha kibali kilichoisha muda wake .....Nusu ya gharama za kibali cha awali

**SEHEMU G**

**ADA ZA KUNUNUA ZABUNI ZA HALMASHURI**

(i) Ukusanyaji wa mapato .....Tshs100,000/=

(ii) Ujenzi wa barabara .....Tshs100, 000/=

(iii) Ukusanyaji na uondoshaji wa Taka ngumu..... Tshs 50,000/=

(iv) Unyonyaji Kupakua mashimo ya maji machafu (vyoo) ..... Tshs50,,000/=

(v) Kurekebisha na kujenga vyoo vya uma, maduka na vioski..... Tshs 70,000/=

(vi) Matengenezo ya mali za Halmashauri (Magari na majengo).....Tshs100,000/=

(vii) Ukaguzi na upimaji wa viwanja..... Tshs100,000/=

(viii) Usimamizi na uendeshaji vyoo vya umma ..... Tshs50,0000/=

(ix) Uendeshaji na usimamizi wa stalls za Halmashauri..... Tshs 50,000/=

(x) Huduma elekezi / mshauri (Consultancy services) .....Tshs 100,000/=

(xi) Maduka / Vizimba ..... Tshs 20,000/=

**SEHEMU H**

**USHURU WA KUGOA VYOMBO VYA USAFIRI VYA MAJINI**

i. Ushuru wa kugesha Mitumbwi.....Tshs 1,000/=kwa siku

**SEHEMU I**

**GHARAMA ZA UNYONYAJI MAJI MACHAFU**

i) Choo cha matumizi ya Nyumbani .....Tshs 60,000/= kwa trip

ii) Vyoo vya Taasisi .....Tshs 150,000/= kwa trip

iii) Vyoo vya Nyumba za kulala wageni

Guest House na maeneo ya Baa na Mighahawa.....Tshs 60,000/= kwa trip

iv) Vyoo kwenye hoteli au Motel .....Tshs 120,000/= kwa trip

v) Vyoo kwenye viwanda ..... Tshs 150,000/= kwa t

## SEHEMU J

### ADA YA VYOO VYA UMMA

i) Ada ya choo na bafu

Haja kubwa .....	Tshs 300/= kwa mara moja
Haja ndogo .....	Tshs 300/= kwa mara moja
Kuoga .....	Tshs 500/- kwa mara moja

## SEHEMU K

### ADA YA USAJILI WA VIKUNDI MBALIMBALI

i. Taasisi zisizo za kiserikali .....	Tshs 30,000/=
ii. Vikundi vya kijamii(CBO).....	Tshs 15,000/=
iii. Vikundi vya ujasiliamali .....	Tshs 15,000/=
iv. Jumuiya za watumiaji maji .....	Tshs 50,000/=
iv. Waganga wa Jadi .....	Tshs 50,000/=

## SEHEMU L

### ADA NA USHURU WA MABASI, DALADALA, MAGARI BINAFSI YANAYOINGIA STENDI YA MABASI

(i) Basi kubwa .....	Tshs. 5,000/=
(ii) Basi dogo(min basi ) .....	Tshs. 3,000/=
(iii)Costa .....	Tshs 2,000/-
(iv)Daladala .....	Tshs 1,000/=
(v) Gari binafsi.....	Tsh. 500/=

22) Sheria hizi zinafuta sheria za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma za mwaka 2010 Tangazo la Serikali Na.259 la Mwaka 2011.

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa imebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kufuata azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kilichofanyika tarehe .....mwezi .....2017 mbele ya:

***MHE. PARTICK WILLIAM GUMBO***  
MSTAHIKI MEYA,  
HALMASHAURI YA MANISPAA  
MUSOMA

.....  
**FIDELICA G .MYOVELLA**  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA  
MUSOMA

**NAKUBALI,**

TAREHE.....  
**DODOMA**

.....  
***MHE: GEORGE B. SIMBACHAWENE (Mb)***  
**WAZIRI WA NCHI – OR - TAMISEMI**